

# MKUHUMI

MKAKATI WA KUPUNGUZA UZALISHAJI WA HEWA YA UKAA INAYOTOKANA NA UKATAJI WA MITI NA UHARIBIFU WA MISITU



Masoud Kipanya

Uharibifu wa misitu ni tatizo la Dunia. Athari zake haziishi kwa mazingira na viumbe hai vinavyotegemea mazingira haya bali pia huchangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya ni tishio kwa sehemu kama Tanzania ambako idadi kubwa ya watu hutegemea mazingira yanayowazunguka. Mabadiliko ya hali ya hewa husababisha madhara mengi yakiwemo mafuriko ya mara mara naukame wa muda mrefu, mvua kunyesha katika nyakati zisizotazamiwa, uwezekano wa kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko na hata kusababisha mazingira ya esili tuliyo nayo leo kupotea kabisa. Kwa kuzingatia athari hizi, Jumuiya ya Kimataifa inaangalia njia za kupunguza tatizo hili na njia mojawapo ni MKUHUMI. Ifuatayo ni hadithi ya msichana REDDA ambaye ana wasiwasi wa kutoweka kwa misitu iliyoko katika kijiji chake na anatafuta mbinu za kuhakikisha ustawi wa misitu kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Hivi karibuni REDDA alikwenda kumtembelea Shengazi yake anayeishi katika kijiji cha mbali. Alipokuwa huko aliona udhuru mkubwa katika suala zima la uhifadhi wa misitu. Miti karibu yote ilikatwa kwa ajili ya mashamba, uvunaji wa magogo na uchomeji wa mkaa. Uharibifu huu wa mazingira umepelekea wakazi wa kijiji cha Shengazi yake REDDA kupata taabu katika



kutafuta kuni, maji safi na hata kujipatia kipato kupitia mbeo, madawa ya asili ufugeji wa nyuki na kadhalika.

Alipokuwa anarudi kutoka kwa Shengazi yake REDDA alipokelewa na mandhari nzuri iliyotokana na misitu iliyozunguka kijiji chao lakini moyo wa REDDA haukuwa na furaha kutokana na aliyoyaona alikotoka.



Naogopa kijiji chetu kisije kikaingia katika tatizo la kukata miti na kupoteza uzuri wa esili

REDDA aliamua kupitia kwa rafiki yake ambaye ni mhitimu wa Chuo Kikuu katika masuala ya misitu. Akamuhadithia yote aliyoyaona.



Nina hofu ya kijiji chetu kuingia katika tatizo la kukata miti na kupoteza faida ambazo misitu huleta kwa jamii inayotunza misitu.

Naiielewa hofu yako REDDA, hivi karibuni nimejifunza kuhusiana na MKUHUMI. Huu ni Mkakati ambao kijiji chetu kinapaswa kutikira kujiunga



Tuitishe mkutano wa kijiji ili tulizungumzie jambo hili.

Kwa msaada wa Serikali ya Kijiji, kikao cha dharura kikaitishwa.

Ndugu wanakijiji naomba tuwasikilize vijana wetu.

REDDA akahadithia yote aliyoyaona katika kijiji cha Shengazi yake.

Kijiji chote kimekuwa kikavu, miti karibu yote imekatwa, sasa hivi inawalazimu kutembea umbali mrefu kufuata kuni na maji kutokana na uharibifu wa misitu. Tumeonelea tuliseme hili ili yanayotokea kule yasije kutokea na hapa kwetu kwa sababu mahitaji yetu na yao hayatofautiani.

Rafiki wa REDDA naye akaendelea...

Wazee wangu nimejitunza mbinu mojawapo tunayoweza kuitumia kutunza misitu yetu...


Na wakati huohuo kupata faida kutoka Jumuiya ya Kimataifa, mpengo huu unaitwa MKUHUMI.

Eheee! Mbona siamini ninachokisikia, hebu tufafanulie.

Habari ndio hiyo, huu ni Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa inayotokana na Ukataji wa miti na Uharibifu wa Misitu. Bado kuna mengi zaidi ya kufahamu kuhusiana na mpengo huu na najua kutakuwa na maswali mengi zaidi kutoka kwenu. Cha msingi ni kwamba uamuzi uko mikononi mwetu kama kijiji, kuukataa au kuukubali na kufaidi matunda yatakayotokana na uhifadhi wa misitu yetu. Tunapaswa kufaham ni kiasi gani cha pesa tutapata na namna kitakavyoweza kutunyanyua kiuchumi.

Ni kweli, hilo ni muhimu sana, hatuwezi kupata faida bila ya kuifanyia kazi. Sasa tunapaswa kufanya nini? Ina maana tukiukubali mpengo huu hatutoweza tena kutumia miti kwa maisha yetu ya kila siku?

Hapana, bado tutaweza kuitumia lakini kwa njia zitakazoepusha uharibifu na kuendeleza ustawi wake. Bado sina maelezo ya kina kuhusiana na taratibu kiujumla lakini ni muhimu jamii yetu ikafahamu kuhusiana na jambo hili kabla ya kufanya uamuzi wa kujiunga na MKUHUMI.



Asanteni sana wazee wangu kwa michango mbalimbali, asante Mwenyekiti kwa ufafanuzi wa kisheria uliutoa. Hii inaonekana kuwa ni nafasi nzuri kwetu kwa sababu tutaweza kunufaika kwa njia nyingi. Kwa usimamizi endelevu wa misitu yetu tutaweza kuendelea kuitumia na kupeta faida na wakati huohuo kuiweka vizuri ili vizazi vijavyo viweze kuikuta ikiwa katika hali nzuri ili nao waweze kuwawekea watakaokuja.



Uko sahihi REDDA, tunapaswa kutafuta mbinu za kutusaidia kutunza misitu yetu. Tunajua kwamba misitu ina umuhimu mkubwa sana kwetu na tuna nia ya dhati kabisa kuihifadhi. Hata hivyo tunapaswa kupata taarifa zaidi kuhusiana na MKUHUMI.

Nakubaliana nawe kabisa, tuendeleo kujitunza zaidi kwa kuuliza maswali mengi zaidi.



Baada ya hapo Mwenyekiti alifunga mkutano na wetu kutawanyika huku kila mmoja akitafakari kuhusiana na MKUHUMI

